

JIMBO KATOLIKI IRINGA
TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI TOSAMAGANGA (TIHAS)



S.L.P 50 TOSAMAGANGA
IRINGA
SIMU: 0769 432 532 (MKUU WA TAASISI)/ 0762 482 704 (MHASIBU)
BARUA PEPE: tosamagangainstitute@gmail.com
TOVUTI: www.tih.as.ac.tz

UTANGULIZI

Tunayofuraha kukuaribisha hatika Tasisi yetu ya Afya na Sayansi Shirikishi Tosamaganga. Taasisi inakuarifu tarehe ya kufungua mwaka mpya wa masomo wa 2022/2023 kwa mkupuo wa mwezi wa tisa itakuwa ni tarehe **15/10/2022**.

MUHIMU

Taasisi pia imefikia maridhiano na serikali ya wanafunzi kusitisha huduma ya chakula kilichokuwa kinatolewa na Taasisi, hivyo wanachuo wetu watajitegemea kwa kununua chakula kwa bei nafuu katika kantini inayopatikana ndani ya Taasisi.

ADA NA MALIPO MENGINE KWA MWAKA WA PILI (2022/2023) KWA KOZI YA
UTABIBU (CLINICAL MEDICINE).

ADA NA MALIPO MENGINE KWA MWAKA 2021-2022.

Na	AWAMU	ADA	MALAZI (Hostel)
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	600,000	BURE
2	Awamu ya pili (mwezi Februari)	500,000	BURE
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	600,000	BURE
4	Awamu ya nne (Mwezi Julai)	500,000	BURE
	JUMLA	2,200,000/=	BURE

NB:

1. Gharama za Ada iliyoainishwa kwenye jedwali ilipwe kwenye Kumbukumbu namba ya malipo (**Control Number**) ya mwanachuo kupitia Benki ya CRDB.
2. Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya uchumi wa Taasisi, Jimbo na Nchi.
3. Ada unaweza kulipa yote au kwa awamu nne kama ilivyoainisha kwenye jedwali
4. Mwanafunzi asipotimiza kulipa ada kwa awamu husika hatapokelewa au atarudishwa nyumbani na akikaa nyumbani kwa muda wa siku 21 na zaidi atapaswa kurudia mwaka.
5. Wale tu ambao wamelipa nusu ya ada ya muhula ndio watakasajiliwa kwenye muhula husika.
6. Ada ikishalipwa hairudishwi.

ADA YA MAZOEZI KWA VITENDO

1. Wanafunzi watafanya mazoezi ya Afya ya Jamii kwa vitendo katika vituo mbalimbali vya afya nje ya chuo. Mazoezi hayo yatafanyika katika muhula wa kwanza kwa muda wa siku 21 na katika kipindi hicho mwanafunzi atajitegemea gharama ya chakula. Gharama ya mazoezi hayo ni **Tsh. 100,000/=**. Mwanafunzi aje nayo mkononi wakati wa kuripoti.

MICHANGO MINGINE

1. Gharama ya mitihani ya mwisho wa muhula wa pili inayoendeshwa na Wizara ya Afya ni **Tshs.150, 000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
2. Ada ya Udhibiti Ubora (Quality Assurance Fee) **Tshs.15, 000/=** Kwa ajili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**NACTVET**), UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
3. Matibabu **Tshs.52,400/=** kwa asiye na bima na kwa mwenye bima afike na bima yake (UJE NA FEDHA MKONONI)
4. Mfuko wa serikali ya wanachuo ni **Tsh 10,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
5. Gharama za marudio ya mtihani (supplementary exam) ni **Tsh. 30,000/=** kwa somo (kwa atakae shindwa fikia wastani) na maombi ya mtihani maalumu (Special sit exam) ni **Tsh. 50,000** kwa kila somo (kwa sababu maalum)

Tunakutakia maandalizi mema na **KARIBU**.

ASANTE

.....
ERICK L. MSEMWA
Mkuu wa Taasisi

